TANGAZO LA SERIKALI NA. 70 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA NDEMBO, KITONGOJI CHA ITETE YA MWAKA 2024.

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Ndembo, Kitongoji cha Itete ya mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.

______

JEDWALI

______

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 588582MS, 8975975KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa KS $57^0$ 45' 56.99 MS kwa umbali wa kilomita 1.17 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 289 yenye majira-nukta 589570MS, 8975352KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS $23^0$ 50' 19.46 MG kwa umbali wa kilomita 0.37 hadi kwenye alama ya mpaka namba B yenye majira-nukta 589418MS, 8975008KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS $89^0$ 18' 04.70 MG kwa umbali wa kilomita 0.33 hadi kwenye alama ya mpaka namba C yenye majira-nukta 589090MS, 8975004KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ $35^0$ 34' 13.84MG kwa umbali wa kilomita 0.21 hadi kwenye alama ya mpaka namba D yenye majira-nukta 588972MS, 8975169KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS $80^0$ 55' 42.61MG kwa umbali wa kilomita 0.12 hadi kwenye alama ya mpaka namba E yenye majira-nukta 588853MS, 8975758KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa KS $58^0$ 18' 49.08 MG kwa umbali wa kilomita 0.28 hadi kwenye alama ya mpaka namba F yenye majira-nukta 588610MS, 8975975KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Magharibi katika uelekeo wa KZ $01^0$ 38' 41.87MG kwa umbali wa kilomita 0.97 hadi kwenye alama ya mpaka namba A yenye majira-nukta 588582MS, 8975975KZ; unapoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*